Mwakavutahigh_school@yahoo.com

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**

SHULE YA SEKONDARI MWAKAVUTA,
S.L.P 116,
**MAKETE.**
**Simu**
**Mkuu wa shule 0754 645 903**
**Makamu wa mkuu wa shule 0765 521677/0763 334898**
**Matroni 0763 495 630 /0758 465 990**
**Patron 0743 621 717**

`

KUMB. NA. MSS/JI/78/34. 17/04/2025

NDUGU MZAZI/MLEZI WA
……………………………………………..
……………………………………………..

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA MWAKAVUTA SEKONDARI MWAKA 2025/2026**

1. **UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano katika shule ya sekondari **Mwakavuta** kulingana na chaguo lako____________

Shule itafunguliwa tarehe 08/07/2025, shule yetu ina tahasusi (Combinations 09) HKL, HGL, HGK,CBG, EGM, PCM, HGFa, HGLi na PCB . Shule ipo wilaya ya Makete Mkoa wa Njombe, Km 27kutoka Makete mjini. Usafiri wa mabasi upo kila siku kuanzia, kutoka Njombe hadi Bulongwa makete nauli kiasi 12,000/=, kutoka Bulongwa mpaka shuleni bodaboda nauli sh. 5,000/=. Mbeya Uyole stand ya UKINGA kupitia Ipelele hadi Shuleni kila siku kwa kutumia magari ya Japanese na magari mengine madogo yapo nauli takribani sh. 15,000/=. Mzazi unatakiwa kuonyesha ushirikiano wa hali ya juu na walimu katika maendeleo ya mwanao kitaaluma,tabia na mwenendo. Uvunjaji wa kanuni na taratibu za shule hautavumiliwa kama vile kumpa mwanao **simu ya mkononi. Tafadhali mwanafunzi akipatikana na simu atarudishwa nyumbani na simu itavunjwa.Haturuhusu kabisa mwanafunzi kuja na simu.** Soma maelekezo yaliyoambatanishwa na barua hii na uyatekeleze kisha jaza fomuzilizoambaanishwa na kuzileta shuleni.

2. **MAHITAJI MUHIMU**

Yafuatayo ni maagizo/mahitaji/michango/na vifaa muhimu ambavyo ni lazima uje navyo siku unapofika hapa shuleni.

**(a) Ream (A4) mbili za karatasi kwa mwaka**

**(b) michango**

i) Uendeshaji wa shule 65,000/=
ii) Tahadhari 5000/=
iii) Nembo 5000/=
iv) Kitambulisho cha shule Tsh. 5,000/=

**michango yote inatakiwa ilipwe awamu ya kwanza , Ambayo jumla yote ni 80,000/= elfu themanini tu**

**<u>MUHIMU</u>: FEDHA HIZI ZOTE ZIINGIZWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE YENYE JINA MWAKAVUTA REVENUE COLLECTION ACCOUNT NAMBA 60401100012 (NMB)**
Andika jina la mwanafunzi unayemlipia. Hatutapokea fedha.Njoo na hiyo BPS hapa shuleni na utakatiwa risiti.

3. **<u>SARE ZA SHULE (WAVULANA)</u>**
   - i) Sweta la rangi **kijani jeshi** (kama inavyoonekana katika kiambatanisho No. 1)
   - ii) T-shirt rangi ya blue yenye kora nyeupe (form six) isiyo na maandishi kama umeshindwa kupata zinapatikana karibu na eneo la shule.
   - iii) Suruali mbili nyeusi .Suruali iwe na mshono wa turnup, celebration na mifuko mitatu mmoja nyuma na mbele miwili.
   - iv) Uje na tai ndefu nyeusi.
   - v) Mashati mawili (2) tetron mikono mirefu yanayoweza kuchomekwa ndani ya suruali uje nayo.
   - vi) Aje na "jazzy" za michezo rangi nyekundu na viatu vya michezojozi moja. Michezo hapa shuleni ni lazima.
   - vii) Shamba dress, Suruali za khaki (2) mbili suruali moja aivae wakati anakuja kuripoti, jambo lakuzingatia ni kwamba mwanafunzi hatakiwi kuja na nguo za nyumbani za ainayoyote ile (tafadhali zingatia hilo). Suruali iwe na mshono wa turnup, celebration na mifuko mitatu mmoja nyuma na mbele miwili. (angalia kiambatanisho no.1)
   - viii) Viatu vya ngozi jozi mbili rangi nyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu.
   - ix) Soksi jozi mbili ndefu nyeusi.
   - x) Track suit 1nyeusi yenye fito nyeupe itavaliwa usiku wakati wa"night preparation".
   - xi) Jacket 1 zito jeusi lenye kofia lisilo na maandishi yoyote kwa ajili baridi, majaketi marefu yanayovuka magoti hayaruhusiwi kabisa.
   - xii) Gloves nyeusi zisizo na maandishi kwa ajili ya baridi (zitavaliwa mwezi wa 7 na 8)
   - xiii) Pull neck nyeusi (kaba shingo)

**4. SARE ZA SHULE (WASICHANA)**

1. Sketi 2 zenye marinda ya kumwaga ndefu zinazovuka magoti 10cm kutoka kwenye magoti rangi ya **kijani CCM** (esteem No. 1) na Suruali mbili rangi ya **kijani CCM** (esteem No. 1)
2. Mashati mawili ya tetron yenye mikono mirefu yanayoweza kuchomekwa ndani ya sketi.
3. Shamba dress Magauni mawili rangi ya damu ya mzee na lightblue, moja avae wakati wa kuja.
4. Jazzy za michezo rangi nyekundu na raba za michezo jozi moja. Michezoni ya lazima.
5. Viatu vya ngozi jozi mbili rangi nyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu.
6. Soksi jozi mbili ndefu nyeupe.
7. Track suit moja nyeusi yenye fito nyeupe itavaliwa wakati wa usiku nightpreparation.
8. Jacket moja zito jeusi lenye kofia lisilo na maandishi yoyote kwa ajili ya baridi, majaketi marefu yanayovuka magoti hayaruhusiwi kabisa.

9. Gloves nyeusi zisizo na maandishi kwa ajili ya baridi.(zitavaliwa mwezi wa saba na wa nane)

10. Pull neck nyeusi (kabashingo) nzito.

11. Tai rangi ya **kijani CCM** (esteem No. 1).

12. Kwa wanafunzi wa kiislamu waje na hijabu nyeupe kwa ajili ya kuvaa darasani wakati wa vipindi, damu ya mzee, nyeusi, light blue hizo zitavaliwa na shamba dress.

13. T- sheti yangi ya blue yenye kora nyeupe (form six ) isiyo na maandishi kama akishindwa kupata zinapatikana karibu na eneo la shule.

14. Sweta rangi ya **kijani jeshi** . Kama inavyoonekana kwenye kiambatanisho No. 1

**5. VIFAA VYA BWENI ( KWA WAVULANA NA WASICHANA)**

a) Godoro la sponchi size ft 2 ½ aje nalo, ukiona usumbufu kubeba zinapatikana jirani na eneo la shule.
b) Mashuka (2) rangi ya light blue (maji ya bahari) na pinki, blanketi zito, mto na foronya ya blue na taulo.
c) Vyombo vya kulia chakula sahani, kijiko na kikombe.
d) Toilet paper, mafuta ya kupaka, dawa ya meno, miswaki, sabuni za kufulia na kuogea,
e) Ndoo mbili za lita 10 zenye mifuniko kwaajili ya matumizi binafsi moja utakabidhi ofisini.
f) Tranka 1 na kufuli imara la kuwekea vifaa binafsi na nguo za shule. Usilete begi ambalo ni rahisi kuchanika.
g) Kwa wasichana waje na taulo za kutosha. (Pedi).
h) Vifaa vya usafi vifuatavyo :- brush za chooni (vishungi) , squeezer, hard broom, soft broom , slesha.

**6. MAWASILIANO YA SHULE**

I) Barua S.L.P 116, MAKETE – NJOMBE:
II) email : mwakavutahigh_school@yahoo.com
**III)** SIMU YA SHULE ya Mkuu na Makamu wa shule **0754 645 903 / 0765521677/0763 334 898.**
**IV)** Website : www.mwakavutasecondaryschool.ac.tz

**<u>MUHIMU</u>**: Ni mwiko kwa mwanafunzi **kumiliki simu** au **LAINI** hapa shuleni. Mwanafunzi akikutwa na vitu hivyo, hatua kali zitachukuliwa. Tumia simu ya shule tu ambayo atakuwa nayo MATRON**- 0758 465 990** PATRON – 0743 621 717

**7. VIFAA VYA KITAALUMA**

I) Daftari counter books 08 kwa ajili ya notes za masomo yake , school bag ni lazima kwa ajili ya kuhifadhia madaftarihayo.
II) Advanced Dictionary kwa wote (Oxford)
III) Wanaochukua Tahasusi yenye Kiswahili waje na kamusi na wanaochukua Tahasusi yenye Geography waje na Atlas.

V) Watakaochukua Tahasusi ya CBG, PCM na PCB waje na vitabu vifuatavyo:-
a) Advanced Biology by Michael Robert PCB & CBG
b) Dissecting kit PCB & CBG
c) Scientific calculator PCM,PCB,CBG & EGM.
d) Koti nyeupe kwaajili ya maabara (Laboratory coat) PCB, CBG& PCM.

**BIOLOGY**

**A) VIFAA**

a) Koti jeupe kwa ajili ya maabara (laboratory coat)
b) Dissecting kit
c) Scientific calculator.

**IDARA YA KISWAHILI**

1. Vitabu vinavyopendekezwa mwanafunzi kuwa navyo (Ziada)
2. Nadharia ya lugha Kiswahili 1 kidato cha tano na sita (Jubeek A. Masebo) toleo jipya.
3. Nadharia ya lugha Kiswahili 1 kidato cha tano, sita na elimu ya juu. (Masuko C. Saluhaya) 2016

**VITABU VYA KIADA – ENGLISH LANGUAGE**

1. Advanced Level English: advanced approach by Nicholous Ashel)
2. language One by Mgonja.
3. Language Two by Mgonja.

**<u>SIMU ZA WALEZI WAO (WALIMU)</u>**

Matron 0758 46 59 90 Patron 0743621717/ 0743431049

7. **<u>MAELEKEZO MUHIMU</u>**

a) Baadhi ya wazazi wamekuwa na tabia ya kutelekeza watoto bila kuwapa mahitaji muhimu na fedha za matumizi wakiwa hapa shuleni hivi kuleta usumbufu kwa shule kwa kuwa omba omba wakifikiri shule ina utaratibu wa kuwa na fedha kituhicho akipo ni jukumu lako mzazi/mlezi kumpa fedha za mahitaji yake kupitia simu za walezi wao matron na patron.

b) Baadhi ya wanafunzi wamekuwa na tabia ya kukataa, kufanya kazi za nje kama usafi wa bweni, kufyeka n.k. shule haitavumilia tabia hiyo. Shule haitakuwa na huruma na mwanafunzi wa aina hii. Mwanafunzi lazima afundishwe Elimu ya kujitegemea. Na hii ndio sera ya taifa letu atafanya kazi zote za shule.

c) **<u>SIMU</u>** ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu shuleni na kutumia vifaa vya muziki na camera shuleni. Mawasiliano yote ni kwa kupitia shule kwa namba tulizoorodhesha. Ni vizuri ukalielewa hili vizuri hatutakuwa na huruma katika suala hili.

Usifike bwenini bila kuripoti ofisi ya Mkuu wa shule au Makamu mkuu wa shule.

d) Bank paying-slips ziwasilishwe kwa mhasibu wa shule hapa Mwakavuta na si kwingine.Hakikisha unapewa stakabadhi. Ahadi za kulipa baadaye hazitasikilizwa.

e) Vazi la shule lazima livaliwe wakati wote wa masomo na kwenye shughuli rasmi. Mavazi ya nyumbani hayaruhusiwi kabisa uwapo shuleni.

f) Maagizo ya fedha ( michango yote) na mahitaji yote muhimu vyote vitakaguliwa mara tu mwanafunzi atakapofika kujiunga na shule hii,visipokamilika mwanafunzi atarudishwa nyumbani kuvifuata.

g) Ni marufuku kuja na kofia, pete na mapambo mengine au mitindo isiyofaaya kunyoa nywele.

h) Hairuhusiwi kufuga nywele na ndevu, muda wote nywele ziwe fupi.Shule inayo saloon.

i) Ikiwezekana mfungulie Akaunti NMB/CRDB atafungua akiwa hapashuleni kwa kushirikiana na Benki ya NMB Makete.

Mzazi ukipigiwa simu na mtu yeyote kuhusu mwanao,hakikisha unawasiliana na shule kabla hujatekeleza kile ulichoambiwa kuhusu mwanao.

**8. AFYA**

Unatakiwa kupima afya yako kabla ya kuripoti shuleni, fomu maalum imeambatanishwa kwa ajili hiyo na utatakiwa kukabidhi fomu hiyo iliyokamilika mara tu ufikapo shuleni. Kama una matatizo ya muda mrefu ya kiafya toa taarifa ufikapo shuleni. Vyeti ni lazima uje navyo kama una matatizo sugu. Shule haina uwezo wa kutoa chakula maalum cha wagonjwa wakudumu. Shule haitavulimilia mwanafunzi anayejisingizia ugonjwa kwa sababu zake binafsi. Fomu ya daktari itatumika katika maamuzi yote.

Mwanafunzi aje na Bima ya Afya kama anayo , ambaye hana anashauriwa kujiunga kwenye Bima za kikaya CHF kwa mwaka.

**9. UHURU WA KUABUDU**

Utaruhusiwa kuabudu kwa kadri ya dini kwa kufuata sheria, ratiba na taratibu za shule na za nchi ingawa tabia ya kubughudhi wengine haitavumiliwa. Ukitaka kubadili dini ukiwa shuleni utatakiwa kuleta uthibitisho wa barua kutoka kwa mzazi wako. Shule yetu ni ya mchanganyiko pia kumbuka serikali haina dini hivyo shule haitakubali kuleta taratibu Fulani ili kubugudhi wengine.

**10. KUBADILI JINA**

Hautaruhusiwa kubadili jina lako litatakiwa kutumika kama lilivyotumika wakati wa mtihani wa kidato cha nne (4) au kama lilivyo kwenye Sel-form yako. Ili kupunguza usumbufu wa usajili katika kipengere hiki mwanafunzi anaporipoti anatakiwa kuja na nakala halisi na si copy ya cheti. Result Slips (original).

**11. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

a) Kuiba
**b)** Kutohudhuria masomo zaidi ya siku 90 (utoro) bila taarifa.
**c)** Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzie, walezi na wakubwa
**d)** Kugoma na kuhamasisha mgomo
**e)** Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi au kumpiga mwalimu
**f)** Uasherati na kujihusisha na mapenzi hapa shuleni
**g)** Kuoa au kuolewa
**h)** Kutembelea majumba ya starehe guest house au hosteli ya wasichana/au wavulana
**i)** Ulevi/madawa ya kulevya (kutumia) au kukutwa nayo.
**j)** Kudharau bendera ya Taifa.
**k)** Kumiliki simu ya mkononi shuleni.
**l)** Kuharibu mali za shule kwa makusudi au kuuza mali za shule.
**m)** Kugoma kufanya kazi halali za shule ambazo ni za kwa manufaa yao na ustawi wao hapa shuleni.
**n)** Kuondoka shule kabla ya muda halali wa serikali na kutohudhuria Baraza la kufungia shule.
**o)** Kujihusisha mapenzi ya jinsi moja.

**LUKA N. MKAKATU**
**MKUU WA SHULE**

**Nakala**
Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
S.L.P 6,
**MAKETE**

NB: Matibabu ya mtoto ni jukumu la mzazi na si la shule.

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**

**SHULE YA SEKONDARI MWAKAVUTA.**

**FOMU YA MAPATANO/KUKUBALI NAFASI YA MASOMO NA KUSOMAKATIKA SHULE HII KIDATO CHA________________________________MWAKA__________**

NB: Kabla ya kusaini soma kwa makini maagizo yote kama hutaridhika basi usifike kabisa. Tafuta shule yoyote Tanzania. Shule haitasikiliza vizingizio vya aina yoyote. pia kama afya yako si nzuri fanya utaratibu na mzazi wako kupata shule nyingine ukiwa huko huko shule haitataka usumbufu wowote. Au **KAMA** unataka masomo ambayo shule hii hayapo wasiliana na wizara ili ubadilishwe huko huko.

JINA LA MWANAFUNZI __________________________________________________________
ANWANI:____________________________________________________________________
MIMI________________________________________________________________________

Nimekubali/sikubali kujiunga na Jamuiya ya shule ya sekondari Mwakavuta. Nimesoma maagizo ya shule kwa makini na kuyaelewa Naahidi kuwa mtiifu na nitazingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Kinyume chake hatua kali zitachukuliwa dhidi yangu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Naahidi kusoma kwa bidii sana masomo yangu na kufaulu mtihani. Sahihi yamwanafunzi itakayotolewa na shule, Mkoa na Taifa.

Tarehe__________________________________

**B. Mzazi/mlezi**

Mimi nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa kwa mtoto wangu nimekubali /sikubali mwanangu achukue nafasi hiyo. Naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu kielimu na kitabia, Naahidi pia kumlipia karo ya shule/fedha za matibabu/na michango mingine mbalimbali iliyoagizwa na shule kwa wakati mwafaka kinyume chake nichukuliwe hatua za kisheria.

Sahihi ya mzazi /mlezi_______________________________________Tarehe____________________

NB: Fomu hii itawekwa kwenye faili lake.

Andika namba ya simu ya mzazi________________________________kwa ajili ya mawasiliano na shule.

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

MWAKAVUTA SECONDARY
SCHOOL,P.O.BOX 116,
**MAKETE.**
DATE________________________

TO THE MEDICAL OFFICER.
________________________
________________________
________________________

**PART A:**
Mr/Mrs/Miss________________________________________________________
Please examines the above named pupil as to her/his physical and mental fitness for a fulltime student in this school. The examination should include the following categories.

1. Hemoglobin: __________________________________________________
2. P.V. bleeding: __________________________________________________
3. Eye sight: __________________________________________________
4. Blood pressure: __________________________________________________
5. Urine for sugar: _________________________________________________
6. Stool for routine examination:_______________________________________
7. Skin, Diseases: _________________________________________________
8. Asthma: ________________________________________________________
9. Leprosy: ________________________________________________________
10. Epilepsy: ________________________________________________________
11. Any deformity: ___________________________________________________
12. Pulmonary tuberculosis: ___________________________________________
13. Neurosis: _______________________________________________________
14. Venereal Diseases: _______________________________________________
15. Other serious Diseases: _____________________________________________

Thank you,


**LUKA N. MKAKATU**
**HEADMASTER**


(To be completed by a Government Medical Officer)

1. I have examined the above named pupil and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for full time schooling.
   OTHER COMMENT:_______________________________________________________
2. 
   Date:______________Name and Signature_______________________________
   Designation_________________________________Official Stamp__________________

KIAMBATANISHO NO. 01

1.. School uniform for girls





2. school uniform for boys





3. school Shamba dress (sare za kuvaa nje ya darasa baada ya masom











